## SEMINA YA WATUMISHI – KURASINI: 23 -25 Oktoba, 2014

**Kutumia mafunzo tunayojifunza**

Mch. Tony alipitia kwa muhtasari masomo yaliyofundishwa mwaka jana. Moja ya somo lililofundishwa ni "Kutiana moyo". Watumishi walipewa nafasi ya kueleza jinsi walivyotekeleza somo hilo kwa vitendo katika makanisa yao. Baada ya maelezo ya watumishi kadhaa, Mwinj. Pamphil Balyasaganda alipewa zawadi ya kitabu kiitwacho……………………………….. Kwa kutekeleza somo hilo vema. Alifanya nini? Alimpongeza mtu aliyejenga choo cha kisasa katika kanisa la AICT – Kinzudi kwa kumwandikia barua ya kutambua mchango wake kwa kanisa. Yule mtu alifurahi kupokea barua ile ambayo hakuitarajia. Baada ya kutoa zawadi hiyo, Mch. Tony aliwatia moyo watumishi waendelee kuwatia moyo waumini wao na makundi mbalimbali yaliyomo kanisani .

**Mjadala kuhusu aina nne za udongo Marko 4: 1-20: Swali – Je, tuna wakristo wa aina hii Kanisani?**

1. Kando ya njia – Hulisikia Neno, mara huja shetani na kuliondoa lile Neno lililopandwa mioyoni mwao.
2. Miamba - Hawa hulisikia Neno, hulipokea kwa furaha, ila hawana mizizi ndani yao, ikitokea dhiki hujikwaa.
3. Miiba – Hulisikia neno na shughuli za dunia na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine hulisonga lile neno na kulifanya lisizae.
4. Udongo ulio mzuri – Hulisikia Neno na kulipokea na kuzaa matunda mmoja thelathini, mmoja sitini na mmoja mia.
5.

**Majibu**: Watumishi wengi walikubaliana kwamba "Watu wa aina zote hizi wapo makanisani kwetu". Waumini wengi wa AICT hupenda kusikiliza kwaya tu na wakati mwingine kwaya zisipokuwepo hawaji kanisani. Waumini wengi hawana mizizi ya imani. Wakipatwa na dhiki, wengi huachana na imani. Tuna waumini waliokariri Neno la Mungu lakini hawana mizizi ya imani. Hawa hawajui hata maana ya kulitumia Neno walilokariri (muda wote ni wachanga kiroho). Viongozi wengi wa kanisa hasa wazee na wahudumu huchaguliwa kwa sababu ya vyeo vyao vya kidunia na si kutokana na sifa za kibiblia. Lakini tunao waumini wachache wanaolisikia Neno la Mungu na kuzaa matunda.

**Maswali 2 ya Msingi**

***1. Kuna mtu yeyote anayeweza kutushirikisha endapo Mungu aliwahi kuzungumza naye kwenye maono?***

Watu mbalimbali walielezea jinsi Mungu alivyozungumza nao kwa njia ya maono.

- **Mch. Charles Sanagu**. Mch. Sanagu alizaliwa na kulelewa katika familia ya watu wasiomjua Kristo. Siku moja mwezi Septemba, 1994 saa 9:00 Alasiri alikuwa akichunga ng'ombe za kwao zapata 400. Kipindi hiki kilikuwa kipindi cha kiangazi. Wakati akitembea alifika kwenye mti mmoja uliokuwa na majani mabichi. Ng'ombe wote walisimama wakilia kwa sauti kubwa wakitamani kula yale majani yaliyokuwa kwenye mti ule. Ghafla akasikia sauti ikisema "Unavyoona ng'ombe hawa wanalia kwa kutamani majani hayo, ndivyo watu wangu walivyo na kiu ya Neno la Mungu". Neno hili liliingia moyoni mwake. Baadaye akachukua hatua ya kwenda kujiunga na chuo cha Biblia. Hadi leo anamtumikia Mungu akiwalisha watu Neno la Mungu.

- **Mch. Joshua Loya**: Kanisani kwake kulitokea vurugu. Watu wakashindwa kuelewana na hawakujua ni nani aliyeanzisha vurugu ile. Mch. Loya akaliomba kanisa liombe ili Mungu amdhihirishe mtu huyo. Wengine waliomba kwa shingo upande, wengine walikataa kuomba na wachache waliomba. Mchungaji akawasisitiza kuwa yeyote atakayepata jibu kutoka kwa Bwana amweleze. Siku moja alikuwa amelala na katika ndoto akamwota mtoto wake amejinyea kwenye kaptra yake. Baada ya ndoto hii, alitafakari sana. Ghafla akasikia sauti ikisema,

"Aliyesababisha vurugu ni mwanao". Akatambua kuwa sauti ile ilikuwa ya Mungu. Akapeleka majibu kanisani na ikaonekana ndivyo ilivyokuwa.

- **Mrs Ndongo**: Siku moja akiwa amelala aliota ndoto akipambana na dubu mkubwa sana. Katika mpambano huo alimrarua huyo dubu. Alipoamka hakujua maana yake; Mungu akamwambia kuwa, kulikuwa na vita kubwa sana iliyokuwa inakuja kwenye utumishi wao lakini Mungu atawafanyia mlango wa kutokea. Akamshirikisha mmewe. Baadaye kulitokea vita kubwa katika utumishi wao kiasi kwamba akasusiwa kuwekewa mikono. Mama huyu alikumbuka maneno aliyoambiwa na Mungu, akaomba. Mungu alitengeneza njia hadi sasa mmewe ni mchungaji na wanaendelea kumtumikia Mungu.

- **Mch. Erasmus Malelo**: Ilipokuwa inakaribia Pasaka ya mwaka 2012, Mch. Malelo alikuwa safarini Bulima –Mkoa wa Simiyu. Akiwa Mwanza alihitaji kukata tiketi ya kurudi Dar es Salaam kwenye ofisi za basi la Super na Jimnisa. Alipooneshwa chati alighairi na kurudi Bulima. Usiku wakati amelala aliliota lile gari limepata ajali njiani. Kesho yake akarudi Mwanza na kukuta lile gari bado lina nafasi za nyuma. Akakata tiketi na akapewa kiti namba 60. Walianza safari alfajiri na mapema. Walipofika Dodoma, wakati yeye amelala, ghafla basi lao liligongana na roli. Alipostuka usingizini alisikia sauti ikisema, "Hili ndilo jambo nililokuwa ninakuonesha". Watu wanane walikufa kwenye ajali hiyo na kwa neema ya Mungu, yeye alipona.

- **Mch. Yunja**: Siku moja wakati amelala, aliota jinsi atakavyofanyiwa kesho. Aliota amekamatwa na Trafiki wakati akiendesha pikipiki mahali fulani. Kulipopambazuka hakujali sana kwani aliamini kuwa ile ilikuwa ni ndoto ya kawaida. Hivyo, akamsindikiza mgeni (Mch. Nyatu) aliyekuwa amemtembelea kwa pikipiki kuelekea stand ya basi. Wakati wa kurudi akakamatwa na Trafiki eneo lile lile aliloota usikuh Haya yalitokea kwa sababu hakuisikiliza sauti yu Mungu.

***2. Katika uzoefu wako, umewahi kumsaidia mwislamu yeyote kuwa Mkristo? Ilikuwaje? Nini kilitokea kwa mtu huyo? Alijiunga na kanisa? Maisha yake yalibadirika?***

- **Mwinj. Salome Risasi**: Amefundisha wengi na hata sasa wamo kanisani. Mwinj, Risasi alisisitiza kuwa wengi hawaijui imani na tusione hofu kuwashuhudia.
- **Mch. Musa Hezron**: Mchungaji alitumia njia ya kumwombea mwislamu aliyekuwa amefungwa katika njia za giza. Alipofunguliwa alijiunga na kanisa. Mch. Hezron alisisitiza kuwa kumshuhudia Mwislamu ni vigumu kuliko kumshuhudia mpagani. Mwislamu anaamini dini yake tu na anaogopa kutengwa na ndugu zake na waislamu wenzake. Lakini ni wajibu wetu kuwashuhudia.
- **Mch. Heri Ruma**: Kabla ya kuokoka, Mch. Ruma aliogopa sana mapepo na uchawi. Baada ya kuokoka mtu wake kwa kwanza kushuhudia alikuwa mwislamu. Wakati huo alikuwa akisoma katika chuo cha DIT Dar es Salaam. Akiwa barabarani alikutana na ndugu mmoja aliyeitwa Ali. Ali alikuwa mwislamu. Baada ya kumshuhudia habari za Yesu alimwomba amwombee. Mch. Ruma aliweka mikono yake juu ya kichwa chake na kuanza kumwombea. Alipoanza kuomba, mapepo yalilipuka na akamwamini Yesu. Hakuweza kujua kama aliendelea kanisani au la.
- **Mch. Emmanuel Masanja**: Mch. Masanja alialikwa kuwa mhubiri katika mkutano wa Injili uliokuwa unafanyika Magomeni. Alipokuwa anahubiri sauti yake iligoma kutoka kabisa. Akatafuta mtu mwingine ambaye angeweza kumsaidia lakini mtu huyo akawa ana udhuru pia. Mtu mmoja akamwombea na sauti ikafunguka. Mwisho wa mkutano ule, waislamu wengi walimwamini Yesu na waliomba mkutano uendelee kwa kuwa walikuwa wanapata amani. Kuna mtu aliyekuwa anatoa mimba mara kwa mara (Mwislamu) ambaye alimpigia simu Mch. Masanja amwombee wakati akiwa labor ili ajifungue salama. Mch. Masanja alimwombea na alijifungua salama. Mch. Masanja alisisitiza kuwa kazi hii ni yetu na hofu isitutawale. Waislamu wengi wanamwitaji Yesu.
- **Mwinj. Moses Mbushi**: Mwaka 2001, timu ya Injili ya watu 10 akiwemo Mwinj. Mbushi ilisafiri kwenda Mwakaje – Zanzibar. Wakiwa pale walitishiwa maisha. Hawakuogopa kwa kuwa walijua wanaye Yesu Kristo katika huduma ile. Walipafa fursa ya kumshuhudia Kristo katika familia ya

mganga wa kienyeji. Wengi waliokuwa wamefungwa na nguvu za giza, Yesu aliwafungua. Usiku yapata saa 8:00, wote walioamini walibatizwa. Kanisa la KKKT likaanzishwa mahali pale. Mwinj. Mbushi alisisitiza kuwa, "Inawezekana kabisa kuwashuhudia waislamu".

- **Mwinj. Yohana Bwire**: Mwinj. Bwire ameshuhudia waislamu wengi na wengi wao wamo kanisani na maisha yao yamebadilika kabisa. Mwinj. Bwire alieleza kuwa, shida inayowapata watumishi wengi ni hofu na kukosa majibu ya msingi ya maswali ya waislamu. Aliendelea kusema kuwa, watumishi wengi hawako tayari kubeba gharama ya kuwasaidia waislamu wanaomwamini Yesu baada ya kutengwa na ndugu zao. "Hii ni changamoto kubwa kwa kanisa" Alisema mwinj. Bwire. Kama tutaweka mfumo na mkakati wa kutekelezeka wa kuwasaidia waislamu wanaotengwa na jamii zao, wapo wengi mmno waliotayari kumwamini Yesu Kristo na kumfanya kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yao.

**Kwa nini kanisa la AICT limechelewa kuyafikia Mataifa mengine na Injili ya Yesu Kristo?**

- Yafuatayo ni majibu yaliyotolewa na watumishi wa AICT chalo cha Dar es Salaam.
- Elimu ndogo ya umisioni
- Viongozi wa ngazi za juu kutoridhia wengine kufanya umisioni nje ya nchi.
- Umaskini na ukosefu wa fedha
- Watu kutojua tafsiri ya Umisioni na mmisionari ni nani? Wengi walijua wamisionari ni wazungu kutoka katika nchi nyingine.
- Kukosa kipaumbele kwa viongozi
- Umisionari kuonekana kama wito wa baadhi ya watu
- Hatukuwa tayari kutumia vipawa na karama za watumishi
- Hatukuwa na mpango wa kutuma wamisionari (kukosa malengo ya kushuhudia nchi nyingine)
- Umisionari kutokuwa kipaumbele cha kanisa
- Wanafunzi wa vyuo vya Biblia kuandaliwa kulea kanisa na si kuanzishaa makanisa.
- Mfumo wa watumishi wa AICT kutumwa na baraza la Utumaji la AICT liliwanyima fursa watumishi kutumika nje ya nchi.

**Je, ni kwa kiasi gani tumefanya umisioni katika maeneo yetu?**

- Kwa kiasi fulani tumefanya umisioni kwani kuna mchanganyiko wa makabila mbalimbali katika kanisa la AICT.
- Wengi wanatii maandiko na wanayafundisha lakini wao hawafanyi. Hata wale waliofundishwa nao hawafanyi kazi za umisioni
- Umisioni sio kwenda nje ya nchi tu. Ni kuanzia nje ya ukuta wa kanisa. Wapo wengi hawajamwamini Yesu katika mazingira tunayoishi.
- Tatizo ni sisi watumishi kutofanya kile tulichoagizwa na Mungu. Ezra alikuwa ameuelekeza moyo wake kusoma, kujifunza, kutenda, na kufundisha.

**Tufanye nini ili kuboresha kazi za misheni katika maeneo yetu na nje ya nchi?**

- Tubadilike kifikra
- Tutii Neno la Mungu na kwenda
- Tuache uzembe . Wengi walipokuwa vyuoni walifanya vizuri katika somo la uinjilisti. Wengi wetu tuna A. Je baada ya kuja utumishini imekuwaje. Tuache uvivu.
- Tuwajibike na kujitoa kwa dhati katika kazi ya Mungu
- Tuache mazoea na mapokeo yasiyo ya kibiblia
- Tukubali kumtii Roho Mtakatifu.